

Maandiko ya faraja kwa wafiwa/ Neno la kufariji wafiwa (*waliopatwa na msiba*).

Ikiwa Mtu kafariki katika Kristo, basi lipo tumaini la kumwona tena..lakini kwa namna moja au nyingine, wafiwa watakuwa katika huzuni kwasababu hawatamwona tena kwa kitambo...hivyo yafuatayo ni maneno machache yanayoweza kuwafaa waliofiwa.

Isaya 41:10 "usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu"

Yoshua 1:9 "Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako".

Yakobo 1:2 "Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu,

mkiangukia katika majaribu mbalimbali;

3 mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi”

Yohana 16:22 “Basi ninyi hivi sasa mna huzuni; lakini mimi nitawaona tena; na mioyo yenu itafurahi, na furaha yenu hakuna awaondoleaye”.

Mathayo 5:4 “Heri wenye huzuni; Maana hao watafarajika”

Zaburi 34:18 “Bwana yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho huwaokoa”.

Zaburi 116:15 “Ina thamani machoni pa Bwana Mauti ya wacha Mungu wake”

Zaburi 73:26 “Mwili wangu na moyo wangu hupunguka, Bali Mungu ni mwamba wa moyo wangu Na sehemu yangu milele”

Warumi 8:18 “Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu”

Ufunuo 21:4 “Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita”

Makala Haya Yanatoa Usafirishaji Wa Bila Malipo Kwa Bidhaa

*Zinazostahiki, [Http://Swisswatch.is](http://Swisswatch.is)
Au Ununue Mtandaoni Na Uchukue
Dukani Leo Katika Idara Ya
Matibabu.*

*2Wakorintho 1:3 Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu
Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote;
4 atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji
wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo,
tunazofarijiwa na Mungu.*

*Yohana 11:25 Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na
uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;
26 naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele.
Je! Unayasadiki hayo?*

1 Wathesalonike 4:13 Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.

14 Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.

Zaburi 147:3 Huwaponya waliopondeka moyo, Na kuziganga jeraha zao

Bwana akubariki.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

MISTARI YA BIBLIA YA FARAJA.

Mistari ya biblia kuhusu maombi.

Je ni kweli Isaka alifarijika kwa kifo cha mamaye? (Mwanzo 24:67).

MAOMBI YA YABESI.

JE! MUNGU NI NANI?

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp